

VITUO VYA MAISHA YA KIROHO

Sisi ni Nani



Huenda unajiona kuwa wa kiroho lakini si wa kidini. Ikiwa ndivyo, Vituo vya Maisha ya Kiroho vinaweza kukusaidia kuchunguza ukuaji wako binafsi wa kiroho. Tunatoa njia mbalimbali za kujifunza zana za kiroho za vitendo zinazofundishwa na falsafa ya Sayansi ya Akili.

Kupitia Vituo vya Maisha ya Kiroho, unaweza kujiunga na jumuiya ya watu wenye mawazo yanayofanana. Tuna zaidi ya vituo 400 pamoja na vikundi vya kufundisha duniani kote. Ikiwa wazo la kujiunga na jumuiya ya wasafiri wenzako linakuvutia, tembelea tovuti www.CSL.org kupata Kituo cha Maisha ya Kiroho kilicho karibu nawe.

SALA YA KISAYANSI

Mbinu yetu ya Sala ya Kisayansi hutofautisha *Sayansi ya Akili* na dini nyingine. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu aina hii ya sala ya uthibitisho kwa njia mbili. Kwanza, unaweza kutembelea *World Ministry of Prayer* mtandaoni au kupitia msaada wa simu. Ukichagua chaguo hili, unaweza kusali pamoja na mhudumu aliyeidhinishwa au kusikiliza sala yaliyorekodiwa yanayoshughulikia changamoto za kawaida. Pata maelezo zaidi kwa kutembelea tovuti www.WorldMinistryofPrayer.org. Pili, unaweza kupata wahudumu waliothibitishwa katika mojawapo ya Vituo vyetu vya Maisha ya Kiroho. Watasali pamoja nawe wakati wa ibada za kawaida au kwa miadi .

ELIMU

Tunashirikisha aina mbalimbali za madarasa katika mazoea ya kiroho, kuvunja vizuizi, historia ya New Thought na uponyaji wa kiroho wa kimetafiziki. Madarasa yapo mtandaoni na kupitia vituo vya karibu. Pia tunatoa programu ya shahada ya uzamili iliyoidhinishwa katika Masomo ya Ufahamu. Shahada hii ya taaluma mchanganyiko inajumuisha utafiti wa kisasa katika nyanja za falsafa, saikolojia, dini, elimu, uongozi, na sayansi na kiroho. Mtu yeyote mwenye shahada ya kwanza iliyoidhinishwa anaweza kuomba kujiunga kupitia tovuti www.HolmesInstitute.org.

MACHAPISHO

Vituo vya Maisha ya Kiroho huchapisha *Guide to Spiritual Living: Science of Mind* jarida la kila mwezi, ambalo limekuwa likichapishwa bila kukoma tangu 1927. Waliosajiliwa wana chaguo la toleo la kuchapishwa au la kidijitali. Pia linauzwa katika maduka ya vitabu, ikiwemo Barnes & Noble, na katika Vituo vya Maisha ya Kiroho vya karibu.

Jarida hili linatoa mada za kisayansi, kifalsafa na kidini za hivi karibuni pamoja na mbinu mbali mbali. Sehemu kuu ni *Daily Guides for Richer Living*, inayotoa msukumo mara 365 kwa mwaka.

Mashirika yetu matatu ya uchapishaji wa vitabu yanatoa aina mbali mbali ya vitabu vya kiroho na kazi za mwanzilishi wetu Ernest Holmes, ikiwemo maandiko yake ya kipekee, *The Science of Mind*. Pata maelezo zaidi katika tovuti www.ScienceofMind.com.

TAARIFA ZAIDI

Kwa maelezo kamili kuhusu vituo vinavyohusika, maeneo ya wanachama, masomo ya mtandaoni yenye ithubati katika *Science of Mind*, maombi ya sala, vitabu, machapisho na fasihi ya bure, tembelea tovuti www.CSL.org au Kituo chako cha Karibu cha Center for Spiritual Living.

